

BENKI KUU YA TANZANIA
16 Barabara ya Jakaya Kikwete
S. L. P. 2303
40184 DODOMA
TANZANIA
Simu: +255 26 2962586



BANK OF TANZANIA
16 Jakaya Kikwete Road
P.O. Box 2303
40184 DODOMA
TANZANIA
Phone: +255 26 2962586

Barua Pepe: botcommunications@bot.go.tz

Email: botcommunications@bot.go.tz

08 Juni, 2022

TAARIFA KWA UMMA

KANUNI ZA FEDHA ZA KIGENI ZA MWAKA 2022

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kuufahamisha umma kuwa Kanuni mpya za Fedha za Kigeni za mwaka 2022, zimetungwa chini ya Sheria ya Fedha za Kigeni, Sura ya 271 kupitia Tangazo la Serikali Na. 294, lililochapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 13 Mei 2022.

Pamoja na mambo mengine, Kanuni hizo zinaruhusu wakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, kuwekeza katika dhamana za Serikali za muda mfupi na mrefu. Aidha, Kanuni hizo zinaruhusu mkazi wa Tanzania kuwekeza katika nchi wanachama wa jumuiya hizo.

Hivyo, Kanuni za Fedha za Kigeni za mwaka 2022 zimefuta Kanuni za Fedha za Kigeni za mwaka 1998 na Kanuni za Fedha za Kigeni (Dhamana zilizoordheshwa katika soko la Hisa) za mwaka 2003. Kanuni za Fedha za Kigeni za mwaka 2022 zinapatikana katika tovuti ya Benki Kuu ya Tanzania www.bot.go.tz.

Prof. Florens D.A.M. Luoga
Gavana
Benki Kuu ya Tanzania

